# Habari za kimataifa
## Waabuduo Damu ya Kristo

Waabuduo Damu ya Kristo – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Rome

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

...Kwa Neno Lako...


Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI - N. 9 - Julai/Agosti 2018


Mhariri

# Msemo wa pekee uliopambwa kwa rangi nyekundu

Hii ni Damu yangu, damu ya agano inayomwagwa kwa ajili ya wengi: huu msemo unaosemwa katika Injili kwenye Karamu ya Mwisho ni moja kati ya ile ambayo haiwezi kuondolewa, na ni mara nyingi tunausikia, kwa sababu ni sehemu ya kumbukumbu. Kwa ishara hiyo ambayo kila wakati inaporejeshwa juu ya madhabahu inathibitisha kuwa Kristo alikufa na alifufuka, ambaye anamwaga damu yake msalabani anatualika "kutoka" na kwenda mbali zaidi kuelekea upendo usio na kipimo ambao ulimgusa Mt. Maria De Mattias na kutugusa sisi dada zake baada ya zaidi ya karne.



Huu ni uzoefu unaogusa moyo, unaohusisha na unaosisimua, unaotusukuma sio kutobaki bila kufanya kitu, bali kuacha mielekeo mibaya ya mapokeo, kutoa maisha yetu bila malipo na bila maslahi na faida binafsi ili kutafuta njia za kukumbatia wakati ujao kwa matumaini, bila kushindwa na kusonga mbele kimyakimya. Hii inamaanisha kutokuwa na hofu ya idadi au kazi, kushinda changamoto za kitamaduni ambazo hutoka katika jamii ya kisasa, ambayo hutufunga katika mfumo wa ubinafsi na kujipendelea. Ni suala la kuhusisha historia, bila kubaki tofauti na kupendekeza upya uinjilishaji ili kutangaza amani na kutenda haki kwa wote.

Mfano wa wanaume na wanawake wengi ambao walitoa maisha yao bila kujibakiza na ambao waliteswa hadi kumwaga damu ili kumtumikia jirani, inatusukuma kujenga Kanisa changa ambalo linafanya watu waonje uzuri wa "furaha" ambayo ina mizizi yake katika "injili ya Heri".

**Sr. Mimma Scalera, ASC**

## Muhutasari


*Mhariri*

Msemo wa pekee uliopambwa kwa rangi nyekundu 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*

Adhimisho la 15 la kumbukumbu ya kutangazwa Mt. Maria De Mattias
Neno la shukrani la Sr. Nadia Coppa 2

Tunasherehekea Utakatifu wa Maria De Mattias 4

…Andariega de Dios 5

*Toka Ulimwengu ASC*

Maadhimisho ya 15 ya kumbukumbu ya Kutangazwa kuwa Mtakatifu Maria De Mattias 7

Maisha ya Mfufuka 8

Tuzo "Sr. Leona Luechtefeld" kwa ajili ya huduma 8

Damu Azizi….Chemchemi hai ya uzima wangu (Shairi) 9

Mizizi ya hatua za elimu ni michungu lakini matunda yake matamu 10

Nyuma ya kuta za gereza: uzinduzi wa kitabu kinachoitwa "L'amore dentro/ Upendo wa ndani" 11
- Kwa mtazamo wa ushuhuda
- Kwa macho ya mwandishi wa habari
- Kwa neno la vijana wahamasishaji

Miaka kumi pamoja na Mtakatifu Maria De Mattias huko Bolesławiec 13

Shukrani kwa Utakatifu wa Maria De Mattias 15

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*

ASC wanaohusika na JPIC – VIVAT wakutana mtandaoni 16

*Ndani ya Shirika*

Kalenda ya Uongozi Mkuu 17

Sherehe za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha 17

Fadi za Kidini 17

Sikukuu za kumbukumbu za nadhiri za kitawa 17

Waliorudi nyumbani kwa Baba 17

# Adhimisho la 15 la kumbukumbu ya kutangazwa Mt. Maria De Mattias Neno la shukrani la Sr. Nadia Coppa

Habari za mchana nyote!

Ni furaha ya kweli kukutana ili kumsherehekea kwa pamoja Maria De Mattias, ambaye tunasikia uwepo wake kama rafiki ambaye “anapenda sana na kuliwazwa” na utakatifu.

Hii sikukuu yetu ni tukio ambalo linatupa fursa ya kujisikia katika umoja kamili uliojengwa kwa Damu ya Kristo. Damu ya Mwanakondoo asiye na waa ambayo Mtakatifu Maria De Mattias alikuwa mfuasi wake, Mwabudu na mtume.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwasalimu nyote na kuwashukuru kwa kweli kwa kupenda kushiriki pamoja nasi furaha ya zawadi ya maisha ya Maria De Mattias na ya karama ya pekee iliyotolewa na Roho kwa Shirika kupitia Yeye.

Tumemsherehekea mwanamke mwenye nguvu, mfanyakazi asiyechoka, kioo cha fadhila za kikristo... Mwanamke mwenye vipaji na aliyejaliwa akili, mwenye upendo na mpole sana, imara na mwenye huruma, mwenye busara na hodari... kupitia hizi kalamu za unyoya imara na safi, Padre John Merlini anatuandikia wasifu wa mwanamke ambaye alijiruhusu abadilishwe na neema awe zawadi kwa wote. Ufahamu wa kina, tunda la uvumilivu, vilimwezesha Pade John kuvuna zawadi za asili na za neema ambazo alitoa Maria De Mattias, mwanamke mpenzi na bibi arusi wa Damu ya Kristo.

Tumemsherehekea Mtakatifu Maria De Mattias kwa sababu alifanya maisha yake kuwa jibu la upendo akiishi kwa ajili ya Mungu ambaye alimtaka mzima kwa ajili yake, na kwa sababu yeye alitaka kuwa wa Mungu bila kujibakiza.

Tayari imepita miaka kumi na mitano tangu hapo 18 Mei 2003, wakati Mtakatifu John Paul II alipomtangaza Maria De Mattias, akitambua ushujaa wa fadhila zake na mtindo wake wa maisha, ule mzizi ambao ulimfanya atangaze Injili. Wengi wetu bado tuna mguso mioyoni wa picha ya Kiwanja cha Mtakatifu Petro uliokuwa umejaa waumini walioshangilia huo utambulisho zizi. Kofia nyingi nyekundu... za waumini wenye kuguswa na wenye shukrani: walioguswa na uzuri wa moyo ambao ulijitoa kwa Neno, juu yake alisimama ili akamilishe hii safari nzuri sana ya utakatifu; wenye shukrani kwa Mungu kwa sababu ya kujitoa kwake kama dada, ambaye kutoka kwake wanachota hekima, wenye shukrani kwa Kanisa ambalo



lilimtambua kama mfano unaostahili kufuatwa.

Huo ulikuwa muda wa neema kwa Shirika zima kwa sababu uliwasha tena ndani yetu sote hamu ya ndani ya utakatifu unaowezekana, wa kawaida, wa siku zote.

Toka miaka kumi na mitano tumesherehekea kumbukumbu tamu ya tukio hilo na zaidi sana utakatifu wa Maria De Mattias, tukimwomba huyu binti wa Vallecorsa msaada ili kujibu wito wa Mungu ambaye anatupenda sana hivi hata kutaka tuwe “watakatifu” kama Yeye alivyo Mtakatifu..., kushiriki asili yake... kuwa warithi wa furaha ileile: umilele. Kama anavyoandika Papa Francisco, “Mungu hasubiri kwamba turidhike na uwepo wa uvuguvugu, hafifu, usio na maana”. Tumeitwa kuruka juu... mbali na taabu ya safari mara nyingi kwenye kilima kwa mzizi wa Injili wa yule anayetaka kumwiga Mpenzi aliyemtafuta sana.

Tunatarajia kwamba jubilei hii itakuwa imewasha tena ndani yetu tamaa ya Mbingu, wakati tunapotembea kwa shauku juu ya dunia hii. kumwelekea Mungu: furaha yetu kuu!

Mtakatifu Maria De Mattias anatutia moyo na anatusindikiza katika safari hii, akituhakikishia kwa maisha yake kwamba inawezekana kuishi Injili hadi ukamilifu wa mabadiliko, na kuwa mfano wa Mpenzi wakati tunapomtumikia katika safari hii ya duniani.

Kwa Maria De Mattia ilitosha kumtazama: Yule Mpenzi; kutoka kwenye mvuto huo zilitoka nguvu nyingi za ndani ... msukumo mkubwa wa kila uchaguzi akipokea mwaliko wa Yesu kuelekea heri, kwenye ile shule ya furaha, maisha ya mafanikio na kipimo cha uwezo wa Mungu.

# Nafasi kwa Uongozi Mkuu

Kwa kuangalia utakatifu wake tunaweza kuelewa kwamba siri ya heri haiko katika kuwa maskini, safi, wapole, bali katika kuwa na uhusiano wa kina na Kristo kiasi cha kubadilisha uwepo na ukweli katika kazi yake. Heri ya Maria De Mattias ilikuwa ile ya kuingia katika uhusiano wa karibu na Bwana wake: alitaka kuwa wake bila kujibakiza ... Alithibitisha kwamba "kwa kiasi ambacho mtu anajitakasa, huzaa kwa ajili ya ulimwengu" (GE 33).

Kila mmoja wetu anaombwa kuingia katika urafiki huu na Kristo ili kujiruhusu kutazamwa na Yeye na kupendwa kama rafiki yake tukiishi vizuri na kukua katika utu kupitia safari iliyojengwa kwa mambo madogomadogo ya kila siku, yale ya upendo na kati ya haya utunzaji na uteteaji wa walio wanyonge zaidi.

Napenda kukumbuka jioni ya leo utakatifu wa kila siku wa masista wengi waliotawanyika duniani kote... utakatifu ule wa masista wanaoshiriki katika kutoa maisha kwa njia ya huduma ya unyenyekevu kwa maskini, kwa waliotengwa, katika maeneo ya pembezoni... wale walioitwa kukabiliana na ufuasi kama uchaguzi unaopingana na desturi na ambao huugharimia kwa miili yao...

Nafikiria utakatifu wa Masista walio na umri mkubwa zaidi ambao wanaoishi kwa ukunjufu na kutolea nyakati za ugonjwa au umri ... utakatifu uliothibitishwa na chungu cha mashaka ya kutokuwa na uhakika ...

Ninakumbuka kwa shukrani bidii na shauku ya majitoleo ya masista walio vijana zaidi ambao wanajifunua kwa ufuasi kwa tamaa kubwa na ambao wanajiruhusu wenyewe kugeuzwa kuwa zawadi kupitia ishara za kawaida, lakini zinazoonekana za kujitoa...

Na kisha, kama si kuona katika uaminifu, kipimo cha kijitoa cha masista ambao wanaishi maisha ya wakfu kama nafasi wazi kwa ajili ya kupokea kilio cha damu ...

Kumbukumbu na mang'amuzi ya utakatifu unaowezekana, wa kawaida... uliojengwa kwa uamini kila siku iliyotumikaa katika kupanda... kila siku iliyotiwa ishara kwa fumbo la pasaka... kutokana na moyo kukutana na Mpenzi ambaye hutuvutia kwake kwa ajili ya uzima.

Mtakatifu Maria De Mattias, utuombee ili mioyo iwake upendo safi, wa kweli kwa ajili ya Bwana... kwa kuwa mara nyingi kwa kupenda tunaweze kupenda.. kwa kawaida tukipenda tunaweza kuuamsha tena ulimwengu. Katika safari hii ya furaha kamilifu na ya kudumu, inatufanya kuwa tayari na wenye uwezo wa kujibu mialiko ya Mungu tukijua kuwa njia ya kwenda mbinguni hupitia dunuani na kwamba maisha ni utume (GE 27).

Napenda kutoa shukrani ya pekee kwa Padre Emanuele, mmisionari wa Damu Azizi ambaye aliongoza Misa hii akiitajirisha kwa tafakari yake na uzoefu wake. Padre Emanuele amefika kutoka kwenye misioni ya watu wengi huko Aversa na ametumegea Neno akitukumbusha kutunza uchaguzi wetu na kutembea kila siku tukitamani ukamilifu wa maisha tunayoyaishi katika Upendo.

Shukrani ya pekee kwa Michele Antoniani, Meya wa Vallecorsa ambaye yupo na kikundi cha vijana ili kutoa heshima kwa Mtakatifu Maria De Mattias. Shukrani kwenu nyote masista kutoka kwenye jumuiya zilizokaribu kwa kuifanya hai hii kumbukumbu na kuifanya kuwa nzuri.



Urafiki wenu uendelee kuwa muungano na uhai kwetu sisi sote.

Heri nyingi za utakatifu kwenu wapendwa masista ziwafikie katika kusheherekea pamoja nasi jubilei hii, kwa washirika wetu, kwenu marafiki, walei wanachama na kwa wote ambao kwa kupitia mfano wa Mtakatifu Maria De Mattias wanafanya kazi kwa shauku ya ndani kufuata nyayo za Mwana Kondoo.

Roma, 18 Mei 2018

**Sr. Nadia Coppa, ASC**
*Mkuu wa Shirika*

# Tusherehekea utakatifu wa Maria De Mattias

Sherehe ya kumbukumbu ya 15 ya kutangazwa Mtakatifu Maria De Mattias imetupa nafasi kuangalia tena maisha yake na utakatifu wake kwa macho ya Kanisa na ulimwengu wa leo.

Hata mawaidha ya Papa Francisco: Furahini na Shangilieni, yanafanana na mwaliko wake kugundua tena na kufanya tena wito wa ubatizo kuendana na utakatifu. Kwa hiyo Uongozi Mkuu ulipenda kutoa siku tatu za tafakari na sala kuhusu utakatifu, kupitia ushuhuda wa Maisha ya Mt. Maria De Mattias.



Jioni ya kwanza ilikuwa na mada wito kuelekea utakatifu wa kila siku, jioni ya pili na ya tatu ziliendeleza mada ile ya wito kuelekea utakatifu wa kimisionari na wito kuelekea furaha ya utakatifu. Nyakati za sala na maadhimisho yalifanyika kwenye Kanisa la Damu Azizi lililoko Largo Pannonia.

Maneno ya masifu na ya shukrani ya Maria De Mattias kwa Damu ya Kristo yalichochea na kuongoza ibada ya kuabudu Mwili na Damu ya Yesu, wakati wa jioni ya kwanza ya sala.

Somo la Injili ya Heri, pamoja na ushuda wa masista kwenye maandamano ya kutangazwa Mtakatifu, yaliboresha jioni ya pili ya sala.

Tarehe 18 Mei, siku ya sikukuu, iliashimishwa mada ya Wito wa kufurahia utakatifu. Mada iliendelezwa na Padre Emanuele Ruggeri, CPPS, ambaye aliongoza adhimisho la Misa. Hata Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, wakati wa kutoa shukrani mwishoni, alishirikisha tafakari yake akiongea juu ya sifa za utakatifu za Maria De Mattias.

Mambo ya maana yalikuwa ni nyakati mbili za burudani mwishoni mwa Misa, maonyesho toka kwa vijana. Kikundi cha kwanza, kile cha vijana wa Vallecorsa, mahali alikozaliwa Mt. Maria De Mattias, kilileta kwa njia ya maonyesho, kwa mtindo wa kisasa, sifa za utu wake. Mchezaji, ambaye alikuwa abeba picha ya Mtakatifu, alifanya ishara, wakati ambapo alikutana na watu waliomfahamu Maria katika maisha yao na ambao waliongea juu yake: baba, mama, Merlini, na mmoja wa wafuasi wake wa kwanza. Na lilitokea wazo la kwanza, jipya la wasifu wa Maria De Mattias. Vijana walieleza sifa za utakatifu wake kupitia rangi za upinde wa mvua.

Kikundi cha pili kilicheza danzi tatu kikitumia nota za nyimbo zilizoandikwa kwa ajili ya Mt. Maria De Mattias katika nyakati za sherehe zilizopita; kilitupatia muda wa sala, kwa madaha kama wasichana walivyocheza na kwa hatua za danzi, walitufahamisha mtiririko na uzuri wa uhusiano wa Mt. Maria De Mattias na Kristo.

Makundi yote mawili yalishuhudia jinsi maisha ya Mwanzilishi yanavyoendelea kuvutia na kujenga sanaa. Maisha yake ni sababu ya mvuto na chombo cha mkusanyiko; mtindo wake safi wa kuishi uhusiano wa Upendo na Yesu kwa ajili ya huduma kwa wale wa mwisho, unaendelea kuuliza na kuita vizazi vipya kwenye maisha thabiti.

**Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC**

## *...Andariega de Dios*

Uzoefu wangu wa kihispania, wa muda mfupi, lakini wa kina, ulipambwa kwa siku za kupendeza na za kuvutia ambapo nilijiachia nisindikizwe na Teresa wa Avila, mhujaji wa Mungu, msafiri mtakatifu na mtembeaji.

Nilifika Madrid manamo tarehe 26 Mei nikiwa na hamu ya kushinda pamoja na masista na kuwafahamu vizuri zaidi, kushiriki maisha yao na kufurahia kazi zao za kitume kati ya watu walio wazi na wabunifu.

Kwenye begi nilibeba hamu kubwa ya kutembea pamoja nao, nikijua kwamba hakuna maisha bila kukutana.

Kuwasili katika jumuiya ilikuwa vizuri sana. Masista wote wa Foundation walikusanyika katika nyumba kuu ili kukaa kwa siku kadhaa pamoja. Tokeo hili la awali limeniwezesha kuelewa hamu ya kukutana, kuwa karibu na kuwa na uhusiano ambao huhuisha mioyo ya hawa Msista.

Tulitumia wiki moja nzima ambapo tulipata muda wa kushirikishana, mazungumzo, sala na utafiti wa pamoja. Hazikukosekana ndoto ambazo zinauweka moyo uhai!

Jumuiya ya Madrid iko makini sana katika kuwapokea kaka na dada ambao wana shida zaidi. Masista pia wanajishughulisha katika kusaidia wakimbizi kwa kuwapa huduma kwenye sehemu ya mapokezi na ya kusikiliza ya parokia. Foundation, licha ya changamoto inazokabiliana nazo, inatafuta namna ya kutoa majibu ya sasa kwa maombi ya nchi; jumuiya ziko makini kupokea katika alama za nyakati, mwaliko wa Mungu, "kuchagua maisha". Uchaguzi wa "walio wanyonge" ni kipaumbele katika utume wa Foundation: wazee, wakimbizi, wafungwa, wanaparokia wanaoishi katika mazingira ya umaskini na hafifu.

Katika mwanga wa maono haya ya sasa na ya ujasiri, kwa miaka kadhaa sasa kituo cha utume kilifunguliwa nje kidogo ya Madrid ambako Waabuduo wanawaweka kwa namna ya pekee watu waliotengwa na maskini kwa msaada wa huduma endelevu wa caritas na nyumba ya wilaya: ishara ya kinabii katika jamii ambayo huelekea kuwatenga na kuwaacha pembeni wadhaifu zaidi, wale ambao kulingana na Papa Francis, huelezwa na utamaduni wa kisasa kama takataka.

Niliweza kutembelea Parokia ya Moyo Mtakatifu ambapo Sr. Pilar kwa miaka amekuwa akifanya kazi ya ufundishaji na akisimamia shughuli na mipango ya kijamii ya wahamiaji. Kwa kweli ni fursa yenye utajiri na shirikishi. Nimegusa kwa mikono shukrani ya maskini ambao hawaachi kubariki kazi ya upendo na ya unyenyekevu ya Sr. Pilar, pia wakiacha kadi za shukrani ambazo nimezipokea kutoka katika mikono ya Paroko kwa shukrani nyingi na kwa fahari.

Jumuiya ya Castuera, ambayo wakati huu sijaitembelea, kwa kweli ni uwepo mzuri katika eneo hilo kwa njia ya umakini kwa wazee




na jumuiya za parokia zinazohitaji huduma ya uchungaji. Mbali na Madrid, eneo hilo hadi magharibi mwa Hispania, jumuiya ya Castuera inaendeleza huduma yake ya unyenyekevu na ya kawaida ya kuwakaribisha wazee ambao, kama ilivyo katika jamii zote zilizoendelea, kwa sasa iko kati ya wale walio pembezoni ikiwatunza na kuwajali. Masista wanaonesha hamu ya kutoa kipaumbele kwa waliodhaifu kama chaguo licha ya changamoto za kila siku wanazokutana nazo.

Ilikuwa vizuri kufurahi pamoja na masista, kukumbuka matukio na maneno ya Pasaka ambayo yalitia alama safari ya maisha yaliyoshirikishwa na utume wa Foundation hii ambayo bado ni hai na yenye ufanisi.

Hispania, taifa linalohusishwa na mila ndogo kama vile Corrida, sangria na flamenco, ni nchi yenye utajiri katika sanaa na historia, yenye mambo ya kiroho ya kina na uzoefu mkubwa wa mafumbo. Nilifurahia kutembelea Makumbusho ya Padro na kustaajabia kazi za bwana Goya na za mchoraji mkubwa Diego Velázquez. Siku za urafiki, za utamaduni, za sanaa, za uzuri ... lakini pia za sala. Nilimalizia muda wangu wa kukaa na safari ya hija huko Avila ... nchi ya Teresa wa Yesù, wa Yohane wa Msalaba.
Nafasi nzuri sana iliyoweka alama safari yangu katika ardhi ya kihispania.

Watakatifu daima wana kitu cha pekee cha kurithisha! Kupitia uzoefu wa ndani wa Teresa wa Yesu nilihisi kuwa na changamoto ya "kutojifurahisha kwa chochote ... bali kutamani yote", kujisukuma kwenye maisha yenye nguvu zaidi na kujitolea kabisa ili kujikuta mwenyewe ndani Yake na kumpata Yeye ndani yangu. Yeye, kama Mume mwenye huruma na mwenye shauku, hakosi kutusaidia kwa uwepo wake wa upendo katika urafiki wa "ngome yetu ya almasi". Teresa wa Yesu alinitia moyo daima kwenda sehemu za pembezoni za miji ... kwenda kukutana na masista kwa moyo ulio wazi na wenye kukaribisha, nakijiachilia kutajirishwa na hekima ya kila mmoja. Sisi sote tunaalikwa kuanza tena safari yetu kila siku, tukijiweka kwa unyenyekevu na kwa upole katika upendo wa Mungu. Katika kujiweka hukoo, kama buu la hariri ambalo linabadilika kuwa kipepeo cheupe, pia maisha yetu yatageuzwa katika maisha yake Yule tumpendaye. .. pamoja, mahujaji wa Mungu!

**Sr. Nadia Coppa, ASC**


Antonio López Olarría
Mª de la Concepción Corral Gómez

Hermosilla, 41
Tel.: 91 576 12 28
28001 Madrid

Todo mi agradecimiento a tan maravillosa Parroquia, que me proporcionó a la persona que cuidó a mi esposo en su enfermedad gracias al buen hacer de SOR PILAR y a todos por su generosidad, cariño y medios para llevar a cabo nuestra despedida.

Siempre

Concha

29/5/2018

Eneo la Bara: Afrika
Region: Tanzania

# Maadhimisho ya 15 ya kumbukumbu ya Kutangazwa kuwa Mtakatifu Maria De Mattias

Jumuiya ASC Manyoni iliadhimisha miaka 15 ya kumbukumbu ya kutangazwa kuwa Mtakatifu Maria De Mattias kwa kumtambulisha kwa watu. Kabla ya siku ya sherehe, masista walifanya tathimini ya maisha ya jumuiya ya mwaka uliopita, namna walivyoishi karama. Waligundua kuwa kulikuwa na hitaji kubwa la kuhamasisha miito, kusali kwa ajili ya Shirika na wagonjwa.



Siku tatu kabla ya sikukuu ya Mt. Maria De Mattias walikuwa na sala na walikuwa na malengo matatu; kusali kwa ajili Shirika, kwa ajili ya miito mitakatifu na kwa ajili ya wagonjwa.

kabla ya tarehe 18, 2018, masista na aspiranti pia walienda kutembelea jumuiya ndogondogo za kikristo na kigango kilichopewa jina la Mwanzilishi wetu na kumwelezea Mtakatifu Maria De Mattias kwa waumini. Watu wengi walishiriki na walifurahi sana kufahamu maisha yake, karama, upendo wake kwa Mungu na kwa jirani wapendwa.

Masista walielezea jinsi Mt. Maria De Mattias alivyogudua upendo wa Mungu usio na mipaka kwa kila mwanadamu, upendo uliojidhihirisha kwa namna ya pekee katika fumbo la mateso ya Krtisto, na jinsi alivyojibu wito wake akijitoa mwenyewe na hatimaye kujiweka wakfu kabisa kwa Kristo.

Maria De Mattias alitambua ndani mwake kuwa, Mungu alikuwa na mpango wa pekee katika maisha yake. Mwezi Machi, tarehe nne, 1834 huko Acuto (Italia) alianzisha Shirika ya Waabuduo Damu ya Kristo ili masista waweze kushiriki katika kazi ya Ukombozi.

Utakatifu ni zawadi ambayo Mungu anatupatia. Kila mmoja ana nafasi kuishi kitakatifu kila siku kupitia wito ambao Mungu amempa. Tunaposherehekea utakatifu wa Maria De Mattias, ni dhahiri kuwa kila mmoja amepewa nafasi ya kuwa mtakatifu.

Watu wote waliopata ujumbe toka kwa masista walifurahi sana na kuhamasika kumwiga huyu mwanamke. Masista waliwapatia picha za Mt. Maria De Mattias ili waziweke katika makanisa yao na katika jumuiya zao.

Siku ya sikukuu, masista, aspiranti na waumini wengine walikuwa na Misa takatifu pamoja asubuhi kwenye Kanisa la Parokia. Jioni masista walikuwa na mlo wa pamoja wakiwemo aspiranti, wamisionari CPPS NA wafanyakazi wa Dispensari ya Mt. Maria De Mattias. wote waliifurahia sikukuu hii na kumshukuru Mungu kwa zawadi ya Mtakatifu wetu.

**Sr. RoseHawa Tantau, ASC**

Eneo la Bara: Amerika
Region Brazili

## Maisha ya Mfufuka

Barua ya hivi karibuni ya Sr. Nadia Coppa kwa ASC, kwa ajili ya kifo cha mama yake mpendwa, imenihamasisha kuandika habari hii kuhusu kaka yangu, Monsignore Geraldo Menezes, padre wa jimbo la Belem, rafiki wa ASC, aliyefariki tarehe 30, Machi mwaka huu, Ijumaa Kuu, kwenye Hospitali ya Bibi yetu wa Guadalupe, akiwa na umri wa miaka 96, miaka 73 aliishi kama padre.

Barua inasema: "Maisha ya Mfufuka ni tumaini la watu wanaopata uzoefu wa mateso".

Kaka yangu alipata huu uzoefu, akichukua ndani mwake matokeo ya shambulio kali kutoka mtu mmoja mbaya miaka thelathini iliyopita, kwenye nyumba ya parokia ya Utatu Mtakatifu ambako alikuwa paroko. Baada ya shambulio hilo la kaka yangu, baada ya miaka ya huzuni, akawa karibu kipofu kabisa, alipata ugonjwa wa Parkison na matatizo mengine mengi. Alikuwa akiishi kwenye nyumba alikozaliwa pamoja na dada wawili, hata wao walikuwa wazee, walimtangulia katika maisha ya milele. Akiwa na ubongo na akili nzuri, alikuwa akisikiliza mziki na habari za ulimwengu na za Kanisa kwenye redio, alipokuwa akiweza aliadhimisha Misa pamoja na padre mwingine na alikuwa akiungamisha.

Geraldo, ambaye aliwafahamu ASC kadhaa na aliowaongoza katika mafungo ya kiroho, aliwapenda Waabuduo, na alikuwa anawashukuru sana kwa kuniruhusu mimi kutoa huduma huko Belam, kwenye jumuiya ya Nyumba ya Merlini, ili kuweza kuwa karibu naye na kumsaidia ilipowezekana.



Daima nilikuwa nikistaajabia mfano wa maisha ya sala ya kaka yangu, mara nyingi alikuwa akiniuliza kuhusu miito yetu, karama na utume wetu, nilikuwa nikimsomea baadhi ya sehemu za gazeti letu ambapo alikuwa anazishika sana.

Nahitimisha nikisema kwamba Geraldo alikuwa akipenda sana Maandiko Matakatifu, kiasi kwamba, katika Kwaresima hiyo, aliniomba nimsomee aya ya Mt. Paulo: "Nakamilisha katika mwili wangu kile kinachopungua katika mateso ya Kristo" (Kol 1:24) baada ya kumaliza kusoma, alisema kwa sauti: Marilia hakuna kinachopungua katika sifa za Kristo. Tunafanya sehemu yetu kwa maumivu zaidi (tukitoa maisha yetu yote kwa furaha na mateso) kwa ajili ya mwili wake, ambao ni Kanisa. Tufanye hayo!".

**Sr. Marília Menezes, ASC**

Region USA

## Tuzo "Sr. Leona Luechtefeld"kwa ajili ya huduma

Mwezi uliopita wanafunzi wawili na mwalimu mmoja wa shule ya Msingi "Shule ya Mt. Theresia wa Salem" huko Illinois, walipokea tuzo zilizopewa jina la Sr. Leona Luechitefeld.

Tuzo zilitangazwa wakati wa adhimisho la Misa ya kufunga mwaka wa masomo tarehe 22 Mei, zilikuwa zawadi za kushangaza kweli kwa Sr. Mary Catherine Clark, ambaye alikaribia kipaza sauti ili kushirikisha watu waliokusanyika maisha ya Sr. Leona na ushuhuda wake wa pekee wa utumishi.

Washindi walikuwa Ryan Wuebbles, wa darasa la pili, Greta Motch, wa darasa la tano na mwalimu wa dini Ann Hilmes, kila mmoja wao alipokea tuzo ya kiasi cha fedha ili naye aweze kuitoa kama mchango.



Bi. Hilmes alitoa tuzo yake kwenye Hospitali ya watoto ya Mt. Yuda, Ryan alitoa tuzo yake kwenye kikundi cha vijana kiitwacho Mioyo Yenye Njaa na Greta alitoa tuzo yake kwanye Hospitali ya Watoto ya Kardinali Glennon.

Tuzo "Sr. Leona Luechtefeld" inaratibiwa na ofisi ya jimbo kwa ajili ya wagonjwa na wazee wa Belleville.

Katika jimbo zima la Belleville wanafunzi waliopokea tuzo walikuwa watatu, ilitolewa kwa ajili ya ujuzi wao jinsi wanavyotafuta namna ya kuishi na kutoa huduma kama wafuasi wa Yesu Kristo.

**Sr. Mary Catherine Clark, ASC**

Eneo la Bara: Asia
Region India

## Damu Azizi….Chemchemi hai ya uzima wangu (Shairi)



Tone kwa tone ...
likibubujika kutoka majeraha matakatifu
Yesu, umenikomboa mimi, kwa Damu yako azizi!
Mpaka tone la mwisho
Bila hofu ya kifo na bila malalamiko
Ulimwaga Damu yako azizi ili kuniokoa.

Ee! Mwokozi Mpenzi! Kondoo uliyechinjwa
Damu yako isiyo na hatia inasambaa juu ya dunia
Upendo wako ni mkuu, mkuu kama joto lako
Kujitoa bila kujipendelea ni asili yako ya upendo.

Hakuna tone la thamani ulilotenga kwa ajili yako
yote kabisa, uliinyunyiza juu yangu
Hatua kwa hatua, ulitembea kuelekea Kalvari
Kokoto za njiani zilichomachoma miguu yako laini.

Nipe "vazi" lako lililolowana kwa damu azizi
Ili niweze kulibusu
Na kisha niponywe, kuimarishwa kwa damu yako
Ee ... Yesu wangu, nisamehe kwa sababu mimi ni mkosefu
Leo na kila siku, kila saa na daima
Niache niishi katika joto la damu yako
Tone kwa tone ... niweze kunywa Kikombe chako cha maumivu
Nitapakwa mafuta na kuwa huru ili kutumikia watu wako.

**Sr. Gracy Vadakumcherry, ASC**

# Mizizi ya hatua za elimu ni michungu lakini matunda yake matamu




*"Unapozingatia lengo lako, unaweza kupata matokeo ambayo haujawahi kufikiri yanawezekana"*
*Catherine Pulsifer*

Tunajivunia kuwashirikisha matokeo yetu ya kitaaluma ya mwaka 2017-18 ...
**Matokeo ya 100% ya Darasa la 10 (ICSE na SSLC).**

Wanafunzi wote wa darasa la 10 wa Chuo cha Aradhana walifikia mafanikio ya lengo la kitaaluma kwa asilimia mia moja, kila mwanafunzi ambaye alifanya mtihani, alifanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo yake na alipitia ndani ya moja ya miaka migumu zaidi ya masomo katika maisha yake .
Bila Shaka, hii isingewezekana bila msaada na majitoleo ya wafanyakazi wetu wanaofundisha! Tunajivunia kitivo chetu ambacho kimesaidia kuimarisha kiwango cha juu cha ubora wa kitaaluma.
Uzoefu huo unathibitisha ukweli kwamba Chuo cha Aradhana kinaendelea kuwekeza katika ukuaji wa akili ya vijana na katika siku zijazo za taifa letu na unatukumbusha kwamba uvumilivu na jitihada hutuzwa daima. Kwa hakika hili linaleta hamasa kwa wanafunzi wajao katika miaka ijayo na ni wakati wa kujivunia na wa furaha kwa kila mwana Aradhana.

**MSHINDI NI ......**
**Chuo cha Aradhana kilikuwa katika nafasi ya 2 katika Jimbo la Karnataka na nafasi ya 10 nchini India**

**Daraja - "Shule za juu 10 zimeorodheshwa nchini India" kulingana na utafiti uliofanywa na Kampuni ya Education Today.**

Shule zimewekwa katika madaraja kwa mujibu wa vigezo tofauti kama: sifa za kitaaluma, umakini wa mtu binafsi, miundombinu, ubunifu wa ufundishaji, usalama na usafi, elimu ya michezo, ubora wa mahusiano, maendeleo ya msingi, ubora wa usimamizi wa uongozi na ushirikiano katika shughuli za kitaaluma, nk. kulingana na tathimini ya wanasheria, kura za wazazi na uchambuzi wa Kampuni EducationToday.
Tuzo ni ushuhuda wa uaminifu wetu na heshima yetu. Uongozi na wafanyakazi wa shule yetu wamejitolea kwa miaka mingi ya kazi kwa wanafunzi wakiwahamasisha kuwa na lengo la juu zaidi. Ingawa tuzo hii ya kifahari imesubiriwa kwa muda mrefu, sisi wa Aradhana tumeheshimika na kuwa na hamasa juu ya kile ambacho tuzo inamaanisha kwetu sisi na kwa kila mwanafunzi.
Tunaona hii kama fursa ya ukuaji zaidi na tunajiwekea malengo ya juu zaidi kwa sababu tunaweza kujiboresha sisi wenyewe katika kufundisha, katika malezi na katika maendeleo mazima ya kila mtoto.

**Chuo cha Aradhana - Bangalore**

Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

# Nyuma ya kuta za gereza: uzinduzi wa kitabu kinachoitwa "L'amore dentro/ Upendo wa ndani"

## Kwa mtazamo wa ushuhuda

Katika gereza kuna siku ambazo zinaweza kujidihirisha: "Daima sawa", lakini leo, Mei 25, 2018 limeandaliwa tukio, ambalo kwa namna ya ajabu limeondoa haya mazingira ya taabu ya siku zote.

Ukumbi wa Taasisi ulijaa, "wa Mwisho", wanaofahamika hivyo katika makundi ya wanaoteseka, walikuwa wanachukua nafasi za kukaa kwa shauku na ukimya kwenye viti vilivyotiwa alama. Jukwaa la mbele lilitengwa kwa ajili ya wageni wa nje, ambao walionesha tabasamu na huruma kwa wote waliokuwepo.

Lilikuwa ni tukio la uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na wafungwa ambao waliongozwa na mfadhili asiyechoka Sr. Emma Zordan, "Mwabuduo Damu ya Kristo", ambaye kwa miaka amekuwa akileta umoja na upendo kwa wote, waliweza kuandika kile ambacho baadaye kimeweza kuwa jina la kitabu "L'amore dentro/ upendo wa ndani".

Kwa wengi kuelezea katika mistari michache hisia hii, ambayo kwa wakati walikuwa wameisahau, inamaanisha kujifunua na kujiacha uchi nafsi yako. Lakini nguvu ya Sr. Emma haina mipaka, aliweza kufanya kiasi kwamba kila mmoja wao, aandike akisikiliza kile ambacho moyo ulimwamuru na bila kujua kwa muujiza gani, kila kitu kilitafsiriwa katika teologia ya hisia ya ajabu na ya kugusa.

... Asante sana kwa wote kwa upendo mlioonesha.

Nawasalimu nikitoa hitimisho langu, lililoandikwa mwishoni mwa utangulizi wa awali kwenye kitabu "Wote tu wa mwisho" na Dk Stefano Ricca, mkurugenzi wa CR, ambaye alikazia mada,



anathibitisha kuwa "wa Kwanza tunaweza kuwa sote": wa kwanza katika umoja, katika usawa, katika tabia, katika uaminifu, katika unyofu, katika kujiamini wenyewe na watu wengine. Wa Kwanza kwa kuzingatia kuwa hakuna "wa Mwisho".

**Giuseppe Medile**

## Kwa macho ya mwandishi wa habari

"Upendo wa Ndani, hili ni jina la kitabu kilichozinduliwa huko Rebibbia, Nyumba ya Wafungwa, tarehe 25 Mei 2018. Hata hivyo yeye Emma Zordan, dada yetu, mwenye nguvu ya ajabu ya asili, kwa miaka amekuwa akifanya kazi za kujitolea, na ni uwepo wa daima na msaada kwa wafungwa. Kitabu hiki kimekusanya mawazo na hisia za wafungwa ambao walichagua kwa uhuru kushiriki katika mpango wa Sista Emma. Upendo daima katikati ya maisha yetu, hisia zisizoweza kukanwa ambapo bila hizo uwepo wetu unakuwa hauzai matunda. Upendo katika hali zake zote, unaooneshwa katika unyenyekevu na ukarimu wa watu ambao daima wako katika kutafuta upendo, labda bila hata kuujua, watu ambao ni wahanga na watenda mbaya kwa wakati mmoja na ambao wanatafuta upatanisho kwa yaliyopita. Watu ambao mara nyingi wanawekwa mbali kama alivyosema Monsignor Petrocchi, Askofu wa Aquila, katika tukio hilo, mtu kubwa na mwenye hekima, ambaye amewashukuru wafungwa kwa fursa ya uzoefu huu.

Mons. Petrocchi meonesha jinsi mtu anavyokuwa na hisia potovu na za taratibu mbaya ambazo humzuia kuona mbele ya ukuta, taratibu zinazo paka chokaa, ni fadhila ya hekima tu inaweza kutupa uwezo wa kujistaajabia katika muundo ambao hatuufikirii. Upendo wa ndani huwasha moto na unatufanya kuona miujiza ya Mungu, na kuwakaribia wafungwa ili kuwasindikiza katika safari yao. Ni katika gereza, watu hupata muda na mahali pa kupata uhuru, kwa sababu wanaweza kuelewa umuhimu na maana ya maisha na mambo ambayo ni muhimu sana. Wafungwa huwa walimu wa kujitegemea kwa sababu wana cha kufundisha watu wote kitu ambacho wanaweza kuepuka wakati wako nje.

Alikuwepo pia Sr. Nadia Coppa, Mama Mkuu wa Shirika ambalo yumo Sr. Emma, ambaye alisisitiza kuwa hakuna maisha bila kukutana na kukutana na walio wanyonge ni mang'amuzi yanayotajirisha. Zawadi utu inatufanya huru kutoka shambulio lolote la vitu vya duniani, na inatupa fursa ya kukutana na Mungu.



Alikuwepo pia Mkurugenzi Dk. Stefano Ricca, Mkurugenzi Msaidizi, Dk. Antonella Grella na wale walioko katika Nyanja ya Elimu. Mkurugenzi ambaye daima anapokea kwa upendo miradi ya kitamaduni, alizawadiwa msalaba kwa niaba ya Shirika zima ASC, kama ishara ya shukrani kwa mapokezi waliyoonesha.

Alikuwepo pia Francesco De Angelis mwanafunzi wa zamani wa Sr. Emma katika nyakati zilizokuwa ngumu zaidi.

Wafungwa wawili Carmine Caiazzo na Giuseppe Medile, kati ya waandishi wa kitabu, walisimulia jinsi kilivyozaliwa kichwa cha kitabu. Halafu waandishi wote walizawadiwa kwa ajili ya uandishi wao.

Mwishoni kulikuwa na igizo kuhusu mada ya unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa makundi ya vijana wa Oratorio " IL GABBIANO" wa Rotondi (AV).

Asanteni Marafiki wa chama "Senza Confini/ Bila Mwisho ambao walishughulikia kipengele cha uchapishaji wa kitabu ambacho karibu chote kilidhaminiwa na Waabudu Damu ya Kristo.

kwa kweli siku ilikuwa ya pekee na ya maana, ambapo zaidi ya maneno, upendo lijionesha na kudhihirika wazi.

**Prof. Maria Teresa Caccavale**

## *Kwa neno la vijana wahamasishaji*

…. Sr. Emma pamoja na Mkurugenzi wa gereza waliandaa sherehe kwa ajili ya uzinduzi wa kitabu na alitamani kuleta uchangamfu, kwa kuwaalika vijana. Bahati iliwaangukia wasichana wetu wa malezi ya mwanzo walio katika hatua ya kujitafiti katika wito na kwa vijana wa Oratori "Il Gabbiano" wa Rotondi.

Aspiranti wanaotaka kujiunga na malezi ya kitawa walitunga na kupiga wimbo katika nota na kuupiga kwa kitaa; wakati vijana wa Rotondi, chini ya uongozi wa vijana wawili: Miriam Sadutto na Antonio Piccolo, daima kwa kutumia nota, waliandaa burudani ya nusu saa katika kuhitimisha sherehe.

Kila kitu kilichotokea katika madhari ya ukimya kilisaidiwa na muziki wa zamani au matamshi ya nyimbo za kiitaliano kikilenga maana ya maisha, matumaini ya kubadili njia, kutokana na kwamba yule aliyeanza safari ameleta uharibifu nje na ndani yake wenyewe.

Matukio, kwa hiyo, yalijieleza kama mapambano kati ya Wema na Uovu unaotafuta kuvutia kwake mawindo. Uovu umejivika weusi, unaonekana kuwa na ushindi na kucheka wakati kijana mmoja, mwenye maisha ya kawaida, anapotekwa. Lakini, hasa katika hali hiyo ya kukosa uhuru, anajisikia kuwa na hisia nyingi tofauti ambazo hupokezana katika moyo wa mfungwa: hasira, hofu, huzuni, chuki, wasiwasi, lakini pia hamu ya furaha, vyote vilionyeshwa na kijana mwenye maski nyeupe.

Katika mabadiliko haya ya hisia, kijana mwenye minyororo huanza kutambua mawazo yake, kutaka uhuru, kubadilisha maisha yake, kuyaonja tayari katika ndoto zake; basi, hapa Wema unajitokeza ukiwa umevaa vazi jeupe ambao, unamkaribia kijana, unapigana na Uovu ambao unarudi nyuma na kuanguka chini ukiwa umeshindwa, wakati huo Wema unafungua minyororo; hisia zinatupa maski na wote wanacheza kwa kuimba wimbo wenye nota: **Kuishi vizuri**.

Matumaini ya kijana yanakuwa ya ukweli. Ndani yake wafungwa walionekana wakiguswa kwa sababu wamewasilishwa vizuri hivi katika hisia zao, na katika mioyo yao, tumaini linapata njia zaidi! Wema unashinda Ubaya! Gereza linaweza kuwa fursa yao kwa ajili ya maumivu ya kupata uongofu na kurudi katika imani ndani ya Mungu anayesamehe na ambaye anataka wawe na furaha ya kweli, kwa njia yake.

Vijana ambao wameweza kuangukia gerezani wanafanya jitihada nyingi katika maandalizi kwa kuchukua muda mbali na majukumu ya kujifunza na kufanya kazi; hofu kubwa ya kuvuka mlango uliozuiliwa na usiokaribiwa; hofu ya kuvuka mlango huo kwa sababu wamezoea kuona kwenye TV wale waliokamatwa; .... Inaanza sherehe ambayo inadumu kwa masaa mawili kati ya mapumziko, ugawaji wa kitabu kwa kila mfungwa na maonyesho ya vijana wetu.



.... Isingewezekana kupata uzoefu zaidi wa kutosha! Utulivu, , kufahamiana kulikojengeka katika nyakati za mapumziko na wakati wa chakula kilichoandaliwa na wafungwa wenyewe kwenye uwanja, kuliacha mguso wa ndani na ulio mzuri.

Vijana wetu waliomba kama wangeweza kuandika kwa wafungwa; wakati wa kurudi walipanga kurudi pia kwenye sehemu zingine za nyumba na kuleta pumzi ya maisha tofauti. Pia waliamua kusimulia hayo mang'amuzi yao kwenye nchi ya Rotondi kupitia maonyesho yale yale na kuwapa watu fursa ya kutafakari juu ya uwazi wa roho katika kuwakaribisha wale watu ambao wameamua kweli kubadili maisha yao.

**Sr. Maria Paniccia, ASC**

*Region Wrocław*

## Miaka kumi pamoja na Mtakatifu Maria De Mattias huko Bolesławiec

Miaka kumi na mitano iliyopita huko Roma, Papa Yohana Paulo wa pili aliweza kumtangaza Maria De Mattias kuwa mtakatifu, Mwanzilishi wa Shirika la Waabuduo Damu ya Kristo. Miaka kumi iliyopita huyu Mtakatifu alitangazwa Msimamizi wa Bolesławiec. Jumapili, Mei 13, ziliazimishwa jubilei mbili.

Sikukuu ya mwaka huu imekuwa na mwelekeo wa kimataifa. Kwenye sherehe hawakualikwa tu waaminifu wa parokia ya Mama wa Mungu wa Msaada wa Daima na wa mji wa Bolesławiec, bali pia walialikwa wawakilishi wa miji miwili ya Italia inayohusishwa na maisha na kazi ya Mtakatifu Maria De Mattias: Acuto na Vallecorsa. Katika Boleslawiec, zaidi ya mameya wa miji hii, walikuja pia vijana, kwaya na umati wa watu pia ulikuja. Waaabuduo pia hawakukosekana, pamoja na Sr. Nadia Coppa Mkuu Mkuu na Sr Wiesława Przybyło, Mshauri Mkuu, ambao walikuja kutoka Italia, na S.r Ewa Kleps, Mkuu wa Region kutoka Wroclaw.

Baada ya kumalizika Vita Kuu ya Pili ya Dunia, miaka 62 iliyopita, Masista wa Kipolandi Waabuduo walifika Bolesławiec pamoja na Wapolandi waliokuwa wakihamia Bosnia ya leo. Kwa njia hii, Bolesławiec ikawa chachu ya maendeleo ya Shirika huko Poland.



Mwanzoni mwa Misa, Sr. Ewa Kleps alielezea mwanzo wa shughuli za masista huko Bolesławiec na Piotr Roman, Meya wa jiji, alizungumza kuhusu jukumu kubwa ambalo maista walifanya katika historia ya maisha baada ya vita ya mji: "Uwepo kwao na kazi yao katika maendeleo ya kiroho na kijamii ulichangia katika uamuzi wa kumchagua kama Msimamizi Mtakatifu Maria De Mattias ".

Sr. Nadia Coppa alisema: "Kuadhimisha jubilei ya mwaka huu ni mwaliko kwetu sisi sote kufanya jitihada za kutambua utakatifu wetu", pia alishukuru jumuiya nzima ya mji kwa msaada ambao masista Waabuduo wamekuwa wakiupokea kwa miaka 62.

Askofu wa Legnica, Zbigniew Kiernikowski, aliyeongoza Misa, alisisitiza kuwa sherehe hii, ibada ya watakatifu, pia ya Mtakatifu Maria De Mattias, na uwepo wa watu kutoka nchi mbalimbali na lugha tofauti, inaonyesha kwamba wote tunatembea katika mwelekeo mmoja na kuongeza kuwa: " Tuombe pamoja ili umbali unaotugawa uwe mdogo iwezekanavyo na kile kinachotuunganisha kiwe na nguvu sana".

Askofu katika mahubiri yake pia alizungumza juu ya fumbo la Kupaa Yesu. Alihimiza watu wote kufanya kazi ya uinjilisti: "Inamaanisha nini kuinjilisha? Kuwa tayari kumwaga damu. Sio mara zote inamaanisha jinsi yanavyosema maneno, lakini kwa kufuata mapenzi ya Mungu, tunapaswa kuwa tayari kupoteza maisha yetu kwa ajili ya wale walio katika uhitaji, tunapaswa kuhubiri ili kujenga umoja na kupigana ili kuwa wakamilifu kadiri ya ukamilifu wa Kristo ", alihitimisha Askofu Zbigniew.

Mwishoni mwa Misa, paroko Stanislaw Kusik aliwajulisha waaminifu kuhusu ombi la parokia na la watu wa mji, kwamba askofu wa Legnica atamtunuku Meya wa Bolesławiec, Piotr Roman, medali ya "Sifa kwa ajili ya jimbo la Legnica". Tuzo hii ni kwa ajili ya kutambua ushirikiano wa manufaa wa Meya na wa mamlaka ya jiji na parokia za Boleslawiec.

Baada ya sala, waaminifu waliweza kuona igizo la Mtakatifu Maria De Mattias lililoandaliwa na wanafunzi wa Shule ya Msingi na vijana wa Vallecorsa na Acuto.

Baada ya sehemu rasmi, kwenye Viwanja vya Boma, ilifanyika sherehe ambapo makundi ya Kipolandi na Kiitaliano yalikutana. Huu mkutano wa kimataifa ulimalizika kwa wimbo wa "Barka".



**Padre Waldemar Wesołowski**

# Shukrani kwa utakatifu wa Maria De Mattias

Mnamo Mei 19, 2018 huko Częstochowa tuliadhimisha miaka kumi na tano ya kutangazwa kuwa mtakatifu Maria De Mattias, tulisherehekea pamoja na waamini wa parokia yetu na marafiki, kumbukumbu ya tukio hili la furaha kwetu sisi sote. Sherehe hii pia ilikuwa fursa ya kukumbuka wasifu wa Mwanzilishi, safari yake kuelekea utakatifu na ujasiri uliokuwepo ndani ya Maria De Mattias katika kumpata mwenzi wa uhakika na yule ambaye ni mtetezi wake katika maisha ya kila siku. Sherehe ilianza na Misa iliyoongozwa na Padre Adam Zyzik, paroko wa parokia ya Mt. Andrea Bobola huko Częstochowa. Mahubiri lakini alitolewa na Padre Władysław Nowak, SDB, ambaye alisisitiza ukuu wa Mt. Maria De Mattias na upendo aliowafundisha vijana na kuwaleta karibu na Kristo. Kwenye sherehe hii walikuja masista kutoka jumuiya ya Bolesławiec na Wrocław na Ungozi wa Region na pia Wamisionari wa Damu Azizi pamoja na Padre Wojciech Czernatowicz, CPPS, Mkuu wa Provinsi.



Baada ya Misa kulikuwa na matukio kadhaa: mashindano ya sanaa ya Maria De Mattias kwa watoto, tamasha la muziki na maonyesho yaliyohusu maisha na shughuli za Mt. Maria De Mattias, michezo kwa ajili ya watoto na tamasha la nyimbo la Bibi Elżbieta Jarząbek. Akiwasalimu watu wote, Bi Elżbieta alisema kwamba tunataka kumwabudu Yesu na kuongeza: "Hatutaki kuwa nyota, bali nota za muziki, kwa sababu hiyo ninamwalika kila mmoja wetu kuwa hii nota ya muziki ili kuimba pamoja masifu kwa Mungu."



Wakati wa sikukuu hii ya furaha kulikuwa na chakula kizuri: nyama zilizochomwa, mikate na matango, sahani za chakula cha moto na vitafunwa vitamu.

Kupitia sala na adhimisho la pamoja tumemshukuru Mungu kwa zawadi ya utakatifu wa Mwanzilishi wetu.

**Sr. Aldona Kala, ASC**

## ASC wanaohusika na JPIC – VIVAT wakutana mtandaoni




*"Kwa mioyo makini kwa kilio cha Damu….. "*
Hati ya Mutano Mkuu 2017

Mnamo Juni 7 hatua ya kwanza ilichukuliwa kwa ajili ya majiundo ya kikundi cha Waabuduo-wanaohusika na JPIC na VIVAT katika Shirika. Yote yalifanyika kupitia mkutano kwenye mtandao kwa njia ya skype ambao uliunganisha masista kutoka Roma hadi Schaan, India, Tanzania, Brazil, Croatia, Marekani, Poland, Argentina, Italia ya Kusini na Hispania ...

Tulizunguka dunia nzima, tukizungumza kwa lugha tatu na kushirikishana habari, mawazo na kicheko.

Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika, alifungua mkutano kwa salamu ya makaribisho na kueleza sababu za mkutano; baada ya muda wa kutafakari kwa sala, washiriki 14 walijitambulisha wenyewe. Kisha Sr. Bridget na Sr. Dani walishirikisha habari kuhusu kazi kupitia mtandao na umuhimu wa kutoa huduma za moja kwa moja, wakikazia umuhimu wa kujifanya wastawishaji wa mabadiliko ya mfumo. Kwa kunukuu mwaliko wa Hati ya Mkutano Mkuu wa 2017, tulishirikishana ndoto ya ASC ya JPIC-VIVAT na sehemu nyingi zinazojumuishwa katika muundo mzima. Yalijadiliwa mawazo ya mpango katika kila Region na Foundation na tulihitimisha kwa kuacha muda mfupi kwa ajili ya maswali na mengineyo. Masista wengi walionyesha shukrani kwa ajili ya mkutano huu na hamu ya kutusaidia sisi Waabuduo popote pale tulipo katika utume kuwa na mwelekeo ule ule wa kujibu kilio cha Damu.

**Sr. Dani Brought, ASC**



## Kalenda ya Uongozi Mkuu




**2-7 Julai** – Mkutano wa kamati ya fedha ASC MDM mikono na moyo
**9 -10 Julai** – Mkutano wa kamati kwa ajili ya marekebisho ya Sheria zetu za Shirika
**12 -13 Julai** – Uongozi Mkuu utakuwa Acuto kwa ajili ya tathimini ya mwaka

## Sherehe za kuzaliwa: Tunasherehekea maisha ya

**Sr. Sheela Mary P.**
03.07.1988 India 30° ya kuzaliwa

**Sr. Caritas Aloyce Kilawe**
10.07.1978 Tanzania 40° ya kuzaliwa

**Sr. Arkandela Brkic**
16.07.1948 Zagreb 70° ya kuzaliwa

**Sr. Mariannina Iannelli**
25.07.1948 Italia 70° ya kuzaliwa

**Sr. Anna Maria Campanaro**
09.07.1938 Italia 80° ya kuzaliwa

## Waliorudi nyumbani kwa Baba



01/06/2018 **Sr. Paolina Ivanković- Piplica** Zagreb
03/06/2018 **Sr. Teresa Trono** Italia
18/06/2018 **Sr. Rosa Corsetti** Italia

## Taaluma ya dini ya kwanza

**29 Julai 2018** - Sr. Jenny Sellaro - USA

## Nadhiri za daima

**22 Julai 2018** - Sr. Nadzieja Raczyckaja– Wrocław

## Sikukuu za Kumbukumbu za nadhiri za kitawa

**Miaka 25° ya nadhiri za kitawa – 15.07.2018**
Sr. Bernadetta Pajdzik Wrocław
**Miaka 50° ya nadhiri za kitawa – 1.07.2018**
Sr. Marieth Walfredo Machado Manaus
Sr. Marian Russo USA
**Miaka 60° ya nadhiri za kitawa – 14.07.2018**
Sr. Jean Marie Kumke USA
Sr. Joan Shalapin USA
Sr. Mary Alan Wurth USA
Sr. Mary Ellen Hubbard USA
Sr. Gabrielle Rowe USA

*Shukrani kwa zawadi ya wito wenu per*


**Habari za kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*

...Kwa Neno Lako...

**Taarifa za kila mwezi**

*iliyorekebishwa na*
***Zinazofamjwa na waabuduo damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI - N. 9 - Julai/Agosti 2018**

*Kamati ya ya waandishi wa habarì*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Inetafsirwa na
*Kikroasia:* ***Sr. Renata Vukadin***
*Kingeraza:* ***Sr. Betty Adams***
*Kiswahili:* ***Sr. Martina Marco***
*Kipolishi:* ***Sr. Bozena Hulisz - Sr. Elisbieta Bukis***
*KIreno:* ***Sr. Clara Albuquerque***
*Kispania:* ***Sr. Miriam Ortiz***
*Kijerumani:* ***Sr. Lisbeth Reichlin***